Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA MAALUM

TOLEO LA JULAI, 2021

## USHIRIKI WA NSSF KATIKA MAONESHO YA 45 YA KIMATAIFA YA BIASHARA YA DAR ES SALAAM (SABASABA)









Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye
NSSF
Simu Bure 0800116773
customercare@nssf.or.tz
@NssfTanzania

# WAZIRI JENISTA AZIPA KONGOLE PSSSF, NSSF KWA UTENDAJI




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama, akiwa katika Banda namba 13 la mashirikiano baina ya NSSF na PSSSF, ili kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa Mifuko hiyo ya Hifadhi ya Jamii. Ambapo alishuhudia namna ambavyo wanachama wa Mifuko hiyo walivyokuwa wakitatuliwa kero zao.

**Na MWANDISHI WETU**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama, amesema katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kumekuwepo na mafanikio makubwa ya kiutendaji ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya PSSSF na NSSF.

Alisema katika kipindi cha siku 100, wanamshukuru Rais Samia kwa sababu wastaafu wengi ambao wanatoka katika Mfuko wa PSSSF, walikuwa wanahangaika kupata mafao yao kwa sababu ya deni, lakini tayari Serikali ya Awamu ya Sita ndani ya kipindi hiki imeonyesha ujasiri wa hali ya juu kwa kutoa Shilingi bilioni 100 ili kuwalipa wastaafu wa Mfuko huo.

Waziri Jenista alisema kwa upande wa Mfuko wa NSSF, katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia unaendelea kufanya vizuri kwa kuongeza makusanyo ya michango inayofikia Shilingi bilioni 100 kutoka bilioni 95 kwa mwezi.

"Hiyo haijawahi kutokea kwa kipindi kirefu cha utendaji kazi wa Mkurugenzi (Mkuu), na Mfuko kwa ujumla, siku 100 za uongozi wa Rais Samia Mfuko wa NSSF umefanya vizuri sana na mimi kama Waziri ninayesimamia mifuko hii najisikia furaha," alisema.

Waziri Jenista alisema thamani ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) hadi kufikia Januari, mwaka huu, imefikia Trilioni 4.8 kutoka Trilioni 3.2 mwaka 2018, lakini kutokana na makusanyo kuongezeka mpaka kufikia bilioni 100 kwa mwezi, thamani ya Mfuko inaanza kuelekea kwenye trilioni 5.2.

# NSSF TUMEELEKEZA NGUVU KUBWA KATIKA KUSAJILI WANACHAMA WAPYA KUTOKA SEKTA BINAFSI NA SEKTA ISIYO RASMI

**Na MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, alisema katika kutimiza malengo waliyopewa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Mfuko umeelekeza nguvu kubwa ya kuwafikia na kuwasajili wanachama wapya kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi pamoja na kukusanya michango.

Mshomba alisema katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia, Mfuko umekuwa kwa kasi sana na kufikia thamani ya Trilioni 4.8 kutoka Shilingi trilioni 3.2, lakini hadi kufikia Juni, mwaka huu, kwa mujibu wa hesabu ambazo hazijakaguliwa thamani ya Mfuko inafikia Trilioni 5.2.

Akizungumzia uboreshaji wa huduma, Mshomba alisema katika ulipaji wa mafao wamefanya kazi nzuri sana na kwa mujibu wa hesabu ambazo hazijakaguliwa za mwaka wa fedha ulioishia Juni, mwaka huu, wamelipa takribani Shilingi bilioni 318, kiwango ambacho ni kikubwa tofauti na miaka ya nyuma.

“Lengo letu siku zijazo si kulipa tu mafao tu, bali ni kuboresha huduma kupitia mifumo mbalimbali ili kurahisisha utoaji wa huduma, kupunguza malalamiko kutoka kwa wanachama na wadau wetu,” alisema.

Aliwakaribisha Watanzania kutembelea banda namba 13 ili waweze kupata huduma zote zinazotolewa na NSSF katika ofisi zake zote nchi mzima, pamoja na kupata elimu ya hifadhi ya jamii.




Afisa Uhusiano Mwandamizi wa NSSF, Rachel Hosea akimhudumia mwanachama alipotembelea banda namba 13 ili kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na NSSF.

# MATUKIO KATIKA PICHA WAZIRI JENISTA ATEMBELEA NSSF, PSSSF




Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Mhagama(katikati), akibadilishana mawazo na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, mara baada ya kutembelea Banda la Ushirikiano linalotumiwa na mifuko hiyo miwili kwenye maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Mhagama (wa pili kushoto) akimsikiliza mwanachama aliyefika katika banda namba 13 ili kupata huduma pamoja na elimu ya Hifadhi ya Jamii inayotolewa na NSSF ambapo pia alipata kujionea jinsi wanachama hao wanavyotatuliwa kero zao.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Mhagama (kulia) akimsikiliza mwanachama baada ya kuhudumiwa na watendaji wa NSSF, katikati ni Afisa Ukaguzi Mwandamizi wa NSSF, Revocatus Kiduli.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama (kulia) akipokea zawadi kutoka kwa Meneja Uhusiano, Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, wakati alipotembelea Banda la mashirikiano baina ya NSSF na PSSSF. Katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba

# NSSF, PSSSF WALIVYO RAHISISHA UTOAJI HUDUMA SABASABA




Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele akihudumia baadhi ya wanachama waliotembelea banda namba 13 la mashirikiano baina ya NSSF na PSSSF.

**Na MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Hosea Kishimba, alisema ushirikiano wa mifuko hiyo kwa kutumia banda moja ili kutoa huduma kumerahisishia utoaji wa huduma kwa wanachama na wastaafu wa mifuko yote miwili kwani wanapata huduma zote eneo moja.

Alisema mifuko hiyo ipo katika banda namba 13 la mashirikiano tokea mwaka 2018, lengo ni kuhakikisha wanafikisha huduma karibu zaidi kwa wanachama na wastaafu bila ya usumbufu.

Alisema walitembelewa na Waziri Jenista ambaye alipongeza namna wanachama na wastaafu wa mifuko hiyo wanavyopatiwa huduma katika banda hilo huku mifuko yote ikiendelea kutoa elimu na kutatua kero za wanachama wao.

Kishimba alisema Alisema kuanzia mwaka 2018, mfuko huo ulipoanzishwa hadi kufikia Juni, mwaka huu, wastaafu 144,000 wamelipwa mafao na Mfuko unalipa pensheni ya kila mwezi shilingi bilioni 58.

# BALOZI ALI IDDI SIWA AFURAHISHWA NA UTOAJI HUDUMA KWA WANACHAMA

**Na MWANDISHI WETU**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Balozi Ali Iddi Siwa, ametembelea banda la Mfuko huo kwenye Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam hivi karibuni na kupongeza maafisa wa Mfuko kwa kazi nzuri ya kutoa elimu na kuwahudumia wanachama.

Alisema katika maonesho hayo yanayofanyika kwenye viwanja vya Julius Nyerere maarufu Sabasaba, amefurahishwa sana kwa jinsi wafanyakazi wa Mfuko wanavyotoa huduma kwa wanachama wanaofika kutafuta huduma mbalimbali na elimu kuhusu mipango ya NSSF kuwapa hifadhi ya Jamii Watanzania hususani wafanyakazi walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

"Katika kupita na kuangalia jinsi huduma zinavyotolewa na maelezo niliyoyapata kutoka kwa maafisa wanaohusika, wapo watu wamefika kwenye banda letu kufuata huduma na wapo waliofika kujiandikisha kwa mara ya kwanza, hii ina maana gani……ina maana kwamba hawa waliofika kujiandikisha wamepata taarifa, wamepata elimu, wameridhika na hatimaye wamejiandikisha." Alisema Balozi Siwa.

Alipongeza hatua za kuboresha mifumo ya TEHAMA kwani katika Mfuko mkubwa kama NSSF mifumo ya kufanya kazi ya kisasa yaani IT ni muhimu sana katika kila jambo.

"Kwa hili naipongeza Menejimenti, Bw. Masha Mshomba pamoja na mwenzake aliyepita Bw. William Erio kwa kuweka misingi na kuhakikisha mifumo hii inastawi na inaendelea kukomaa na hivyo kunakuwepo na uhakika wa Mfuko kukusanya Michango, kuitunza, kulipa Mafao na kuwekeza ile ziada ili kutunisha Mfuko uweze kufanya kazi zake vizuri sana." Alifafanua.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Balozi Ali Iddi Siwa, akimkabidhi kadi ya uanachama wa Mfuko huo Bw. James Adrian Luhimbo ambaye ni mjasiriamali aliyetembelea banda la Mfuko huo kwenye maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwenye viwanja vya Julius Nyerere maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

# HABARI KATIKA PICHA MWENYEKITI WA BODI YA WADHAMINI WA NSSF ALIPOTEMBELEA SABASABA




Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Balozi Ali Iddi Siwa, akimkabidhi kadi ya uanachama, Bw. James Adrian Luhimbo ambaye ni mjasiriamali aliyetembelea banda la Mfuko huo kwenye maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwenye viwanja vya Julius Nyerere maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam Julai 12, 2021




Balozi Siwa akizungumza jambo mbele ya Afisa Mwandamizi TEHAMA, Bi. Rukia Zuberi wakati alipotembelea banda la NSSF. Balozi Siwa alipongeza maendeleo makubwa ya matumizi ya TEHAMA ambayo Mfuko umefikia kwa sasa, ambapo Mwanachama wa NSSF anaweza kupata huduma mbalimbali kupitia tovuti ya Mfuko kwa kutumia simu janja au kompyuta akiwa mahala popote na wakati wowote.



Balozi Siwa (kulia) akizungumza jambo wakati akipatiwa maelezo na Afisa Mwandamizi wa Uwekezaji, NSSF, John Sikoni (kushoto).




Balozi Siwa akishuhudia jinsi Mwanachama (aliyekaa) akihudumiwa na Bi.Stella Kabyemera (kushoto), Afisa Uendeshaji Mkuu, NSSF, wakati alipofika kwenye banda la Mfuko kupata huduma.



Balozi Siwa akiwa na Meneja Uhusiano NSSF, Bi. Lulu Mengele wakati akijionea utoaji huduma kwa wanachama wa Mfuko huo kwenye banda namba 13 la Ushirikiano kwenye maonesho ya Sabasaba.

# MKURUGENZI MKUU WA NSSF NDANI YA SABASABA



Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (katikati) akiwa na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma NSSF, Lulu Mengele (kushoto) akifafanua jambo kwa Mwanasheria wa NSSF Theresia Mponzi.




Mkurugenzi Mkuu NSSF, Masha Mshomba (kulia) akipata ufafanuzi kuhusu mifumo mbalimbali ya TEHAMA inavyowasaidia wanachama wa NSSF kutoka kwa Afisa Mwandamizi TEHAMA wa Mfuko huo Rukia Zuberi.




Mkurugenzi Mkuu NSSF, Bw. Masha Mshomba (wapili kushoto) na Mkurugenzi Mkuu PSSSF, Hosea Kashimba (wapili kulia) wakiwa katika Picha ya pamoja na Mameneja Uhusiano wa mifuko hiyo miwili, James Mlowe (kulia) na Lulu Mengele (kushoto).



Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (kushoto) akipata ufafanuzi kutoka kwa Afisa Miliki Mwandamizi wa NSSF, John Sikoni (kulia) kuhusu miradi mbalimbali ya uwekezaji inayofanywa na Mfuko huo.




Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (kushoto) akipokea ufafanuzi juu ya taratibu mbalimbali zinazotumika kuandikisha wanachama na zoezi la utoaji vitambulisho kwa wanachama, kutoka kwa Afisa Uandikishaji wa NSSF, Edna Rupia (kulia).

# WANACHAMA WA NSSF WAKIPATIWA HUDUMA SABASABA


















MAONESHO YA 45 YA SABASABA - 2021

***Wanachama na wadau wa NSSF walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi wakipatiwa huduma mbalimbali za Hifadhi ya Jamii walipotembelea banda namba 13 katika Maonesho ya 45 ya SabaSaba.***

BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF